## Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara (FAQs)

**Je, mpango wa Better Futures ni nini?**
JBS USA na Pilgrim's zinakuza Better Futures kuwa mpango mkubwa zaidi wa karo ya mafundisho ya chuo ya bila malipo ndani ya Marekani ya vijijini na kuwapatia washiriki wa timu yetu na wategemezi wao fursa ya kufuatilia ndoto zao za elimu ya juu (shahada za ushirika, vyeti vya taaluma) bila karo ya mafundisho.

**Je, kwa nini Kampuni inatoa Mpango wa Better Futures?**
Mpango wa Better Futures unaafikiana na dhamira yetu ya kuunda fursa ya mustakabali bora kwa ajili ya washiriki wa timu yetu. Tunaamini kwamba vyuo vya jamii na shule za kiufundi huwapatia washiriki wa timu na wategemezi fursa ya kujifunza, kuendelea na kukua wanaposhughulika kutimiza malengo yao ya siku zijazo.

**Je, mpango una vipindi vya mafunzo vingapi (credits)?**
Mpango una hadi vipindi 15 kwa kila muhula na hadi vipindi 30 kwa mwaka, kukiwa na kikomo cha jumla ya vipindi 60 kwa mpango (au gharama inayolingana ya kozi zisizo za vipindi vyenye alama za kufuzu chuoni).

**Je, gharama yangu inatarajiwa kuwa gani?**
Wanafunzi wa Mpango wa Better Futures wanapaswa kutarajia kulipa hadi $500 kwa mwaka kwa karo za jumla na vitabu. Kampuni hulipia gharama zote za mafundisho na karo fulani za jumla ili kufanya gharama za jumla za kila mwanafunzi kuwa za chini. Kando na karo za jumla na vitabu, wanafunzi wa Mpango wa Better Futures wanaweza kuwa na gharama fulani za ziada zinazotofautiana kulingana na eneo na shule (ikiwa ni pamoja na karo za kozi maalum, karo za maabara, vibali vya maegesho, n.k). Shule yako mshirika inaweza kukusaidia kukadiria gharama kulingana na programu yako ya shahada, ukubwa wa sehemu za kozi, na wasifu wa usaidizi wa kifedha.

**Je, FAFSA ni nini?**
Idara ya Elimu ya Marekani (U.S. Department of Education) hutumia fomu ya FAFSA (Ombi la Bila Malipo la Usaidizi wa Wanafunzi wa Shirikisho) ili kubainisha ustahiki wa mwanafunzi kupata usaidizi wa kifedha wa shirikisho unaotegemea mahitaji kwa ajili ya chuo kulingana na hali yake ya kifedha. Usaidizi huu unaweza kujumuisha ruzuku na ufadhili wa masomo wa shirikisho, jimbo, na serikali ya mtaa husika.

**Je, kwa nini ninahitajika kujaza FAFSA?**
Tunawahitaji wanafunzi wa Mpango wa Better Futures wajaze FAFSA ili kusaidia kupunguza gharama ya elimu kwa kila mwanafunzi. Kwa kujaza FAFSA, unaweza kustahiki usaidizi ambao hautagharamia tu gharama za karo na vitabu, lakini pia unaweza kusaidia kulipia gharama nyingine za elimu (ikiwa ni pamoja na teknolojia, karo za kozi maalum, usafiri, vifaa, nk). Kati ya usaidizi wa kampuni na usaidizi wowote wa kifedha unaopokea, elimu yako ya chuo cha jamii au cha kiufundi inaweza kuwa ya bila malipo kabisa!

Katika hali ambapo mwanafunzi hastahiki FAFSA, tafadhali wasiliana na betterfutures@jbssa.com ili kujadili machaguo ya kutumia msaada huo.

**Je, Mpango hushirikiana vipi na usaidizi mwingine wa kifedha?**
Mpango wa Better Futures huendeshwa kama mtindo wa ufadhili wa kulipia gharama zinazosalia baada ya ufadhili wa serikali ili kusaidia kupunguza gharama ya chuo ili kutoa uzoefu wa kutolipa karo ya mafundisho. Kampuni

imejitolea kutoa huduma maalum kwa kila mwanafunzi, na hulipa salio linalobaki la karo ya mafundisho baada ya ruzuku na ufadhili wa masomo wa shirikisho, jimbo na serikali ya mtaa kutumiwa.

**Je, ni washiriki wangapi wa timu au wategemezi wanaweza kutumia msaada huu kwa wakati mahususi?**
Ushiriki umewekewa kikomo kwa mtegemezi au mshiriki mmoja wa timu, kwa kila mshiriki wa timu, kwa wakati wowote mahususi. Washiriki wa timu wanaotimiza masharti ya kustahili walio na wategemezi wengi wanaweza kutumia msaada zaidi ya mara moja, lakini mpango unaweza tu kutumiwa na mtegemezi mmoja kwa wakati mmoja.

**Je, itakuwaje ikiwa mume au mke/mwenzi wangu hufanya kazi katika Kampuni pia? Je, sote wawili tunaweza kutumia msaada huo?**
Kila mshiriki wa timu anaweza kutumia msaada huo kwa ajili yake mwenyewe au mtegemezi mmoja kwa kila muhula.

**Je, kuna kozi maalum ambazo mimi au mtegemezi wangu tunatakiwa kujifunza?**
Hapana. Washiriki wa timu na wategemezi wanaweza kuchagua kozi au programu zozote za shahada wanazotaka.

**Je, itakuwaje ikiwa hakuna Chuo cha Jamii au cha Kiufundi karibu na mimi?**
Ikiwa hakuna shule washirika karibu na kituo cha kazi au washiriki wa timu hawawezi kutumia msaada ana kwa ana, washiriki wa timu wataelekezwa kwa Chuo cha Rio Salado, mshirika wetu ambaye ni chuo cha mtandaoni.

**Je, ninaweza kuhudhuria mafunzo ya kozi nikiwa zamu kazini?**
Washiriki wa timu hawatapewa idhini ya muda wa mapumziko wakati wa zamu zao za kazi ili kuhudhuria mafunzo au kufanya shughuli za kozi. Mshiriki yeyote wa timu anayetaka kutumia Mpango wa Better Futures sharti apange kufanya hivyo nje ya zamu zake za kazi.

**Je, itakuwaje ikiwa mtegemezi wangu au mimi nitajiandikisha katika masomo ya muda maalum (part time)? Je, mtegemezi wa ziada anaweza kutumia sehemu iliyosalia ya msaada kwa muhula kama wangu?**
Hapana. Msaada unapatikana tu kwa mshiriki mmoja wa timu au mtegemezi mmoja kwa kila muhula, bila kujali hali ya uandikishaji ya mwanafunzi huyo.

**Je, nini hufanyika nikikoma kuwa mfanyakazi wa Kampuni katikati ya muhula?**
Iwapo mshiriki wa timu atakoma kuwa mfanyakazi wa Kampuni katikati ya muhula, Mwanafunzi(Wanafunzi) Anayetimiza Masharti ya Kustahili ataruhusiwa kukamilisha muhula huo katika Mpango, lakini hatastahiki kwa msaada baada ya hapo.

**Je, Kampuni ilichagua vyuo washirika vipi?**
Washiriki wa timu ya Rasilimali Watu kutoka JBS USA na Pilgrim's walichagua vyuo washirika kulingana na mahusiano ya awali kati ya vituo vya kazi na vyuo, na ukaribu na vituo vyetu vya kazi ili kusaidia kuimarisha kujitolea kwetu kwa mpango wa Hometown Strong.

Tumejitolea kutoa uwekezaji muhimu ambao una athari ya kudumu katika jamii zetu kwa ajili ya vizazi vijavyo. Katika hali hii, uwekezaji wetu unafanywa katika mustakabali wa washiriki wa timu yetu na familia zao, pamoja na vyuo washirika.

**Je, ninaweza kushiriki katika Mpango wa Better Futures ndani ya muda gani baada ya kuanza kufanyia Kampuni kazi?**
Mpango wa Better Futures hutoa karo ya mafundisho katika chuo cha jamii au shule ya ufundi bila malipo kwa mshiriki yeyote wa timu au mtegemezi ambaye ni mtoto wa mshiriki wa timu ambaye:

- Ana mwenendo mwema,
- Ameajiriwa muda wote na Kampuni kwa miezi sita iliyopita,
- Ana mshahara wa msingi usiozidi $130,000 kwa mwaka, na
- Ataendelea kuwa mwajiriwa wa Kampuni wakati wa muhula wa chuo cha jamii wa mtegemezi au mshiriki wa timu

**Je, JBS USA na Pilgrim’s zitalipa chuo mshirika vipi?**
Chuo mshirika kitaipatia Kampuni ankara moja kwa moja kwa karo za mafundisho za kila muhula, na Kampuni italipa chuo mshirika moja kwa moja kwa gharama za jumla za mafundisho kwa ajili ya wanafunzi wowote wa Better Futures wanaotumia msaada katika chuo hicho mshirika.

**Je, itachukua Kampuni muda gani kulipa ankara?**
Mara nyingi, Kampuni italipa ankara siku 30 baada ya kuipokea.

**Je, naweza kutumia mpango huu kwa wajukuu wangu?**
Ikiwa mshiriki wa timu ni mtunzaji wa pekee wa wajukuu wake, wajukuu huchukuliwa kuwa wategemezi wanaostahiki kwa msaada huo. Washiriki wa timu wataombwa kutoa ithibati ya kuwa watunzaji wa pekee katika hali hizi.

**Je, itakuwaje ikiwa ninaishi katika jimbo tofauti na chuo mshirika cha kiwanda changu?**
Endapo mshiriki wa timu ni mkazi wa jimbo tofauti na chuo mshirika cha kiwanda chake, mshiriki wa timu au mtoto mtegemezi lazima atumie chaguo la mshirika wa mtandaoni wa Chuo cha Rio Salado.

**Je una maswali zaidi?** Tafadhali wasiliana na Better Futures Program – BetterFutures@jbssa.com.

- - -

**Nyenzo**
Unatakiwa kujaza Ombi la Bila Malipo la Usaidizi wa Wanafunzi wa Shirikisho (FAFSA®) ili uweze kustahili kwa usaidizi wa kifedha wa kusaidia kulipia gharama za chuo: fafsa.gov

Mpango wa Better Futures haulipiwi ushuru kwa washiriki wa timu, lakini huenda ushuru ukatozwa kwa watoto wategemezi. Tunapendekeza utafute ushauri kutoka kwa msaidizi wako wa utayarishaji wa ushuru ili kuelewa dhima ya ushuru inayowezekana kwa matumizi ya msaada ya mtegemezi.